# مُخْتَصَرُ أَحْكَامِ زَكَاةِ الفِطْرِ

# MUHTASARI WA HUMUKU ZA ZAKAAT AL-FITR

## Maana yake:

Zakaat al-Fitr ni sadaka anayotoa mtu kwa sababu ya kuruhusiwa kula mchana, baada ya kumalizika swaumu ya mwezi wa Ramadhani.

## Hukumu yake:

Zakaat al-Fitr ni wajibu kutoa kwa kila muislamu; mwanamme au mwanamke, mkubwa au mtoto mdogo, muungwana au mtumwa.

Kwa hadithi ya Ibn Omar رَضِيَ عَنْهُمَا amesema: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amefaradhisha Zakaat al-Fitr pishi ya tende au shairi, juu ya mtumwa na muungwana, mwanamme na mwanamke, mdogo na mkubwa miongoni mwa waislamu"[1].**

## Je, Zakaat al-Fitr imefaradhishwa mwaka gani?

Imefaradhishwa Zakaat al-Fitr katika mwezi wa sha'bani, mwaka wa pili hijria (tangu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ kuhamia madina).

## Ni ipi hekima ya kufaradhishwa kwake?

Kutoka kwa Ibn Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amefaradhisha Zakaat al-Fitr kwa ajili ya kumtwaharisha mfungaji kutokana na maneno machafu na upuuzi, na kwa ajili ya kuwa ni chakula kwa masikini"[2].**

Na amesema Ibn Uthaymin رَحِمَهُ اللهُ :

**"Sababu ya kutoa kwake ni kudhihirisha shukrani juu ya neema za Allaah Ta'alaa juu ya mja wake, kwa kuruhusiwa kula mchana baada ya kukamilisha saumu ya ramadhani"[3].**

---

[1]- Bukhari (1503) na Muslim (984)
[2]- Abu Daud (1609) na Ibn Maajah (1827)
[3]- Al-Fataawa (Jz. 18, Uk. 257).

## Masharti ya mtu anayepasa kutoa Zakaat al-Fitr ni mawili

1. Awe muislamu
2. Awe ana chakula cha ziada ya kile kinachomtosha yeye na familia yake, katika mchana wa siku ya Eid na usiku wake.

## Je, mtoto mdogo mwenye mali anaweza kujitolea Zakaat al-Fitr?

Amesema Imam Shaukani -Allaah amrehemu-:

**"Inapasa Zakaat al-Fitr ya mtoto mdogo kutoka kwenye mali yake ikiwa anayo mali, na kama hana itapasa juu ya yule anayesimamia matumizi yake"[(4)].** Na hukumu ni kama hivyo kwa Mwenda wazimu.

## Je mwana wa matumboni (mimba) inatolewa Zakaat al-Fitr?

Amesema Ibn Qudama -Allaah amrehemu-:

**"قَالَ ابْنُ الْمُنْذِرِ: كُلُّ مَنْ نَحْفَظُ عَنْهُ مِنْ عُلَمَاءِ الْأَمْصَارِ لَا يُوجِبُونَ عَلَى الرَّجُلِ زَكَاةَ الْفِطْرِ عَنْ الْجَنِينِ فِي بَطْنِ أُمِّهِ"**

**"Amesema Ibnul Mundhir: Maulamaa wote wa miji ambao tumehifadhi kutoka kwao elimu, hakuna anayesema ni wajibu kwa mtu kumtolea Zakaat al-Fitr mwana wa matumboni (mimba)"[(5)].**

## Je, ni sharti kwa mtu anayetoa kumiliki kiwango maalumu?

Hakuna dalili yenye kufahamisha kwamba mtu anatakiwa kumiliki kiwango maalumu ili aweze kutoa Zakaat al-Fitr, tafauti na zaka ya mali ambayo inashurutishwa mtu kumiliki kiwango fulani cha mali ili uweze kutoa, ndiyo maana maulamaa wanataja sharti la mtu kuwa muislamu na kupata ziada ya chakula chake yeye na familia yake katika mchana wa Eid na usiku wake, atatoa kiasi cha kilo 2 na nusu ya chakula kinachopendwa zaidi katika mji wake.

Amesema Imam Shaukani -Allaah amrehemu-: **"Dalili za kisheria zimelifungua (jambo lake), wala hazijamhusisha tajiri au masikini"[(6)].**

---

4- Nailul Autwwari (Jz. 4, Uk. 214).

5- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 99), mas'ala namba: (1991).

6- Nailul Autwaar (Jz. 4, Uk. 251).

## JE ITAFAA KUTOA KIASI CHA PESA BADALA YA CHAKULA?

Kuna khilafu baina ya maulamaa, na wengi wanao wanaona kwamba haifai kutoa pesa n.k badali ya chakula, na ndio msimamo wa maimamu wanne isipokuwa Abu Hanifa رَحِمَهُ الله .

Amesema Imam Malik -Allaah amrehemu:

"وَلَا يُجْزِئُ الرَّجُلَ أَنْ يُعْطِيَ مَكَانَ زَكَاةِ الْفِطْرِ عَرْضًا مِنَ الْعُرُوضِ"

**"Wala haitoshelezi kwa mtu kutoa pesa katika Zakaat al-Fitr"[7].**

Kadhaalika Imam Al-Maawardi' -Allaah amrehemu- amesema:

"وَلَا يَجُوزُ إِخْرَاجُ الْقِيمَةِ فِي زَكَاةِ الْفِطْرِ"

**"Wala hairuhusiwi kutoa thamani (pesa n.k) katika Zakaat al-Fitr"[8].**

Amesema Sheikh Ibn Baaz Allaah amrehemu: **"Kauli ya maulamaa wengi ni kwamba, wajibu ni kutoa chakula, na hiyo ndiyo kauli sahihi"[9].**

Amesema sheikh Ibn Uthaymiin -Allaah amridhie-: **"Kauli sahihi ni kwamba haifai katika Zakaat al-Fitr kutoa kiasi cha pesa badali ya chakula". [Al-Fataawa] (Jz. 18, Uk. 265).**

## NI WAKATI GANI ITATOLEWA ZAKAATUL FITRI?

Kuna wakati wa kujuzu, nao ni siku moja au mbili kabla ya kumalizika mwezi wa ramadhani, kwa kumkabidhi mwenye kusimamia Zakaat al-Fitr, na wakati wa wajibu, amba oni baada ya kuzama jua siku ya mwisho ya ramadhani, na wakati ulio bora zaidi ni asubuhi ya siku ya Eid kabla ya kwenda kuswali: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amefaradhisha Zakaat al-Fitr... na ameamrisha itolewe kabla watu hawajatoka kwenda kuswali". [Bukhari] (1503) na [Muslim] (986).**

Lau mtu alisilimu au mtoto alizaliwa siku ya mwisho ya Ramadhani, muda mchache kabla ya kuzama jua, itampasa kutoa Zakaatul fitr, na wala haifai kutoa baada ya swala ya Eid, kwa hadithi inayosema:

---

[7]- Al-Mudawwana (Uk. 392)

[8]- Al-Haawil Kabiir (Jz. 3, Uk. 383)

[9]- Al-Fataawa (Jz. 15, Uk. 287)

«مَنْ أَدَّاهَا قَبْلَ الصَّلَاةِ، فَهِيَ زَكَاةٌ مَقْبُولَةٌ، وَمَنْ أَدَّاهَا بَعْدَ الصَّلَاةِ، فَهِيَ صَدَقَةٌ مِنَ الصَّدَقَاتِ»

**"Aliyetoa kabla ya swala hiyo ni zaka iliyokubaliwa, na aliyetoa baada ya swala hiyo ni sawa na sadaka nyingine (haina malipo ya zakatil-Fitr)"[10].**

## MAMBO MBALIMBALI KUHUSU ZAKAAT AL-FITR:

1. Hapewi Zakaat al-Fitr isipokuwa masikini tena muislamu.
2. Inafaa kumfanya mtu wakala kwa ajili ya kutoa Zakaatul fitri.
3. Inafaa kwa masikini kuwakilisha katika kupokea Zakat al-Fitri.
4. Hakuna dua maalumu ya kusoma wakati wa kutoa.
5. Zakaat al-Fitri hutolewa katika sehemu ambayo itakupata sikukuu ya Iddi, hata kama ni mbali na mji wako.
6. Inajuzu kumtolea Zakaat al-Fitri mtumishi wako wa ndani akiwa ni muislamu, na asili ni kuwa atoe yeye mwenyewe.
7. Haifai kumpatia mtumishi wako ila akiwa ni masikini.
8. Inafaa kwa mtu aliyepewa Zakaat al-Fitri kutoa kumpa mtu mwingine anastahiki, endapo yeye amepata chenye kumtosheleza na ziada, pia anaruhusiwa kuuza akihitajia hilo.
9. Akichelewa kutoa Zakaat al-Fitri kwa udhuru au kwa sababu ya kukosa masikini wa kumpatia atatoa akipata wepesi wa hilo.
10. Itafaa kumpa Zakaat al-Fitri masikini mmoja hata kama ni chakula cha watu wengi.
11. Mwenye kutoa Zakaat al-Fitri baada ya swala ya Iddi, haitazingatiwa na itakuwa ni sawa na sadaka nyingine.
12. Akichelewa kutoa Zakaat al-Fitri kwa makusudi, atapata dhambi na itamlazimu yeye kulipa.
13. Itafaa kumpatia msimamizi anayekusanya Zakaat al-Fitri kwa siku moja au mbili kabla ya kumalizika ramadhani.

**Namuomba Allaah aturuzuku Ikhlaas katika kauli na amali zetu.**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**
**Alkhamis ya 30/ramadhani/1447h - 19/03/2026m**

---

[10]- Abu Daud (1909)